DAMU YA KRISTO

MTO WA REHEMA

YALIYOMO

UTANGULIZI **4**
MTO WA REHEMA, UTUOKOE **5**
BILA YA KUSALI SALA HAZIJIBIWI **6**
DAMU YA KRISTO KATIKA AGANO JIPYA **7**
MAISHA YETU **8**
WIMBO KWA HESHIMA YA DAMU TAKATIFU **9**
LITANIA ZA DAMU TAKATIFU **10**
MATOLEO SABA **12**
KUJIWEKA WAKFU KWA DAMU YA YESU **14**
MISA YAKE NA YETU **16**
ROZARI YA DAMU AZIZI YA YESU **17**
NJIA FUPI YA KUSALI ROZARI YA DAMU TAKATIFU **23**
NOVENA YA DAMU AZIZI **25**
KUSHIRIKI DAMU YA KRISTO **27**
SALA KWA MARIA, MAMA WA DAMU AZIZI **29**
SALA KWA MTAKATIFU GASPARI KUOMBA UPENDO KWA DAMU TAKATIFU **31**
SALA KWA MTAKATIFU GASPARI KWA AJILI YA KANISA **32**
SALA KWA MTAKATIFU FRANSISKO XAVERI **33**
SALA KWA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS **34**
SALA YA MTUMISHI WA MUNGU YOHANE MERLINI KWA AJILI YA SHIRIKA **35**
SALA YA KUMWOMBEA MTUMISHI WA MUNGU YOHANE MERLINI KUTANGAZWA MTAKATIFU. **37**
SALA KWA AJILI YA MAHITAJI YA SHIRIKA **38**
HISTORIA FUPI YA MAISHA YA MTAKATIFU GASPARI DEL BUFALO **39**
HISTORIA FUPI YA MAISHA YA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS **43**
BABA YETU **44**
MANENO YA USHUHUDA **45**

THE CATHOLIC DIOCESE OF DODOMA

Bishop's House
P.O. Box 922
Dodoma

23rd Feb. 2007

BPD/Prot.Nr .65\2007

Fr. Felix Mushobozi C.PP.S
Tanzania Vicariate
P. O. Box 932
DODOMA

Mheshimiwa Fr. Mushobozi,

Yah.: Idhini ya Kuchapisha Kitabu cha Sala "Mto wa Rehema":

Ninakutakia amani ya Kristu :Mkombozi wetu.

Tafadhali husika na mada iliyodokezwa hapo juu. Baada ya kuupita muswada wa kitabu husika, ninaafiki kwamba ni cha manufaaa makubwa ya kiroho siyo tu kwa wanashirika bali hata kwa waamini kwa ujumla. Kwa msingi huo, ninaruhusu kichapishwe.

Wenu Katika Kristu,

+Thaddaeus S. Ruwa'ichi OFMCap
Askofu wa Dodoma.

UTANGULIZI

Lengo la kitabu hiki ni kueneza ibada ya Damu Takatifu ya Yesu Kristo na kumuenzi Mtakatifu Gaspari, mtume hodari wa Damu ya Kristo. Kama alivyosema yeye mwenyewe, “Mafumbo yote ya imani yanaunganishwa katika thamani hii kubwa ya wokovu wetu”.

Kitabu hiki kinachapishwa upya kwa mara nyingine baada ya kukifanyia marekebisho madogomadogo na kuongeza baadhi ya sala muhimu.

Pamoja na sala yapo pia maelezo mafupi ya maisha ya Mtakatifu Gaspari na ya Mtakatifu Maria de Mattias.

MTO WA REHEMA, UTUOKOE

Kanisa huita Damu ya Kristo, “Mto wa Rehema.” Tunataka kuuendea mto huu, pamoja na wale wote wanaojisikia fukara, wagonjwa, wenye matatizo na waliosahauliwa…, kwa kuomba msaada, neema, mwanga na faraja.

Tunawaalika pia wale wajisikiao furaha na amani, kuimba pamoja nasi utukufu na shukrani, kwa kuwa Yesu Kristo kwa Damu yake alitukomboa na kutuletea pendo la Baba yake.

Tusaidiane, katika sala za binafsi, au za vikundi, kugundua fahari ya imani na mapenzi ya Mungu, ambaye hutufanya watu wapya.

Katika ibada ya Damu Takatifu ya Yesu, tunataka kumtolea Mungu damu, inayomwagika kutokana na mateso tunayokutana nayo, kama sadaka kwa wokovu wa ulimwengu; tukiwa tayari hata kutoa damu yetu, yaani maisha yetu, kwa utukufu wa Bwana na ukombozi wa watu.

BILA YA KUSALI SALA HAZIJIBIWI

Maisha bila lengo ni tasa;
Hakuna kitakachopatikana bila kuwa na lengo.
Na mtu ni mashine tu kama hana roho.
Tusipozituma meli nje, hazitarudi bandarini.
Na pasipo mashindano, mshindi hatakuwepo...
Kwani huwezi kushinda michezo bila kushindana.
Vivyo hivyo, sala hazitajibiwa bila ya kuzisali vizuri.
Hivyo, chochote kinachohuzunisha maisha yako leo,
Kitapata ufumbuzi wake ukipiga magoti na kusali.
Usisali kwa burudiko au afya yako,
Wala kwa heshima, sifa au utajiri wako,
Bali kwa lengo la kufanya kuishi kwako kuwe na thamani.
Sali kwa kujitoa, kwa furaha na bila ubahili,
Kwani raha yako itakuwa kuu
Na nono zawadi yako
Unapofanya lengo la maisha yako kumchagua Mungu.

Helen Steiner Rice

DAMU YA KRISTO KATIKA AGANO JIPYA

Mathayo 26-27

Kisha akatwaa kikombe, akamshukuru Mungu, akawapa akisema: “Kunyweni nyote, maana hii ni Damu yangu inayothibitisha agano, damu inayomwagwa kwa ajili ya kuwaondolea watu dhambi” (Rejea Mt. 26: 27-28).
Haifai kuziweka katika hazina ya Hekalu kwa maana ni fedha ya damu (Rejea Mt. 27:6).
Ndiyo maana mpaka leo shamba hilo linaitwa shamba la damu (Rejea Mt. 27:8).
Mimi sina lawama juu ya kifo cha mtu huyu; shauri yenu wenyewe! Watu wote wakasema: damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu (Rejea Mt. 27:24).

Wakolosai 1:19-20

Maana Mungu mwenyewe aliamua kwamba Mwana anao ukamilifu wote wa kimungu ndani yake. Basi kwa njia yake, Mungu aliamua kuupatanisha ulimwengu wote naye. Kwa Damu ya Kristo msalabani Mungu alifanya amani, na hivyo akavipatanisha naye vitu vyote duniani na mbinguni.

1 Petro 1:18-19

Maana ninyi mnajua kwamba mlikombolewa katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliupokea kutoka kwa wazee wenu, si kwa vitu vyenye kuharibika: kwa fedha na dhahabu; bali mlikombolewa kwa Damu ya thamani ya Kristo, ambaye alikuwa kama mwana kondoo asiye na dosari wala doa.

Ufunuo 5:9-10a

Basi waliimba wimbo huu mpya: “Wewe unastahili kukitwaa hicho kitabu na kuivunja mihuri yake. Kwa sababu wewe umechinjwa, na kwa damu yako umemnunulia Mungu watu kutoka kila kabila, lugha, jamaa na taifa.
Wewe umewafanya wawe ufalme wa makuhani wamtumikie Mungu wetu nao watatawala duniani”.

Rejea nyingine:

Mt.27: 25; Mk.14: 24; Lk.22: 44; Yoh.6: 53-56; 19:34; Rm.3: 25; 1Kor.10: 16; Ef.1: 7; Ebr.9: 13; 1Yoh.1: 7; Uf.1: 5; 7:14.

Ee Baba wa milele, nakutolea Damu Takatifu ya Yesu kwa msamaha wa dhambi zangu, kwa ajili ya roho za watu waliopo toharani na kwa mahitaji ya Kanisa lako lote Takatifu. Amina

MAISHA YETU

Maisha yetu yote yatolewe
kwa ajili ya Mungu,
ambaye alitupenda hata akawa kwetu
shahidi wa upendo na Mwokozi:
alitupenda na akatuosha katika Damu yake

(Rej. Uf. 1: 5).

Hii ndiyo namna ya kuleta

juu yetu na juu ya wengine

katika ukweli na undani

baraka ya Damu Takatifu ya Mwokozi;

turudie kwa ajili hii
maneno ya mtume:
nasaidia kukamilisha
kile kilichopungua bado
katika mateso ya Kristo.
Nasi tukimbilie kila mara
katika madonda matakatifu
ya Bwana wetu Yesu Kristo,
nayo yatakuwa mapumziko yetu
na amani yetu.

Mt. Gaspari Del Bufalo

WIMBO KWA HESHIMA YA DAMU TAKATIFU

Enyi watu wote, pigeni makofi,
mwimbieni Bwana kwa sauti ya furaha
na shangwe,
kwa kuwa Mungu aliye juu na mwenye uwezo,
ametuonyesha rehema zake.
Kwa kuwa hakumng'ang'ania mwanawe,
bali alimtoa kwa ajili yetu
ili atukomboe kwa Damu yake
na atufanye huru toka dhambi zetu.
Na hivyo tukihesabiwa haki katika Damu yake,
tuokolewe kutoka hasira ya Mungu Baba kwa njia yake.
Na sisi tuliokuwa tumetengana naye,
tupatanishwe kwa njia ya Damu ya Mwanawe.
Ee Bwana, Mungu wangu, nitakurudishia nini
kwa mema yote uliyonikirimia?
Nitachukua kikombe cha wokovu,
na nitaomba baraka ya Damu hiyo.
Mwimbieni Yesu, enyi watakatifu wake wote,
na mtangaze kumbukumbu ya utakatifu wake,
kwa kuuwa alitupenda na kutuosha kwa damu yake,
Na amekuwa kwetu msaada na mkombozi.
Itukuzwe milele Damu ya Kristo
aliyetufanyia maajabu hayo.
Ahimidiwe Yesu milele,
mbingu na dunia zijae utukufu wa Damu yake. Amina.

Njooni tumwabudu Kristo, Mwana wa Mungu,
aliyetukomboa kwa Damu yake.

Mtakatifu Maria De Mattias

LITANIA ZA DAMU TAKATIFU

Bwana, utuhurumie.....Bwana utuhurumie
Kristo, utuhurumie.....Kristo utuhurumie
Bwana, utuhurumie.....Bwana utuhurumie
Kristo, utusikie.....Kristo utuhurumie
Kristo, utusikilize.....Kristo utuhurumie
Baba wa mbinguni, Mungu, ***Utuhurumie***
Mwana mkombozi wa ulimwengu, Mungu, „
Roho Mtakatifu, Mungu „
Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja .....”
Damu ya Kristo, Mwana wa pekee wa
Baba wa milele, ***Itukomboe***
Damu ya Kristo, Neno la Mungu aliyejifanya mtu, „
Damu ya Kristo, ya Agano jipya na la milele, „
Damu ya Kristo, iliyotona ulipotoa jasho la damu, „
Damu ya Kristo,iliyotoka ulipopigwa mijeledi, „
Damu ya Kristo, iliyotoka ulipovikwa taji la miiba, „
Damu ya Kristo, iliyomwagika msalabani, „
Damu ya Kristo, thamani ya wokovu wetu, „
Damu ya Kristo, asili ya maondoleo ya dhambi, „
Damu ya Kristo, kinywaji na kiosha roho, katika Ekaristi, „
Damu ya Kristo, mto wa rehema, „
Damu ya Kristo, mshinda mashetani, „
Damu ya Kristo, nguvu ya waungama dini, „
Damu ya Kristo, kinga ya walio hatarini, „
Damu ya Kristo, shime ya wasumbukao, „
Damu ya Kristo, tulizo la wenye uchungu, „

Damu ya Kristo, tumaini la wanaotubu, ***Itukomboe***

Damu ya Kristo, faraja ya wanaozimia, „

Damu ya Kristo, amani na furaha ya mioyo, „

Damu ya Kristo, amana ya uzima wa milele, „

Damu ya Kristo, yenye kuziokoa roho toharani, „

Damu ya Kristo, inayostahili utukufu na sifa zote, „

Mwana Kondoo wa Mungu, uondoaye dhambi za dunia, utusamehe, Bwana.

Mwana Kondoo wa Mungu, uondoaye dhambi za dunia, utusikilize, Bwana.

Mwana Kondoo wa Mungu, uondoaye dhambi za dunia, utuhurumie.

K. Ee, Bwana, umetukomboa kwa Damu yako.

W. Na ukatufanya kuwa Ufalme kwa Mungu wetu.

Tuombe

Ee Baba, uliyekomboa ulimwengu kwa Damu Takatifu ya Mwanao wa pekee, utunze ndani yetu wokovu uliotupatia kwa rehema yako ili tunapoadhimisha mafumbo matakatifu hayo tupate daima manufaa ya wokovu wetu. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

“Tuwe na upendo kwa Kristo msulibiwa moyoni mwetu na tujitahidi kumfahamisha kwa wengine ili wote wapate kumpenda.”

Mtakatifu Maria De Mattias.

MATOLEO SABA

1. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani, na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa utukufu wa jina lako takatifu, kwa ujio wa ufalme wako na kwa wokovu wa watu wote.

Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, Kama mwanzo na sasa na siku zote na milele, Amina.

Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu aliyetukomboa kwa Damu yake.

2. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa uenezaji wa Kanisa lako, kwa Baba Mtakatifu, Maaskofu, Mapadre, Wamisionari, Watawa na kwa utakatifu wa Waamini wote wa Taifa la Mungu.

Atukuzwe…
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu…

3. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa uongofu wa wakosefu, kwa itikio la neno lako na kwa umoja wa wakristu wote.

Atukuzwe…
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu...

4. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa viongozi wa Umma, kwa ajili ya uadilifu na kwa amani na usawa kati ya mataifa.

Atukuzwe…
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu…

5 . Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa kutakatifuza kazi na mateso ya watu, kwa maskini, wagonjwa, wenye taabu, na kwa wale wanaotegemea sala zetu.

Atukuzwe…
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu…

6. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa ajili ya haki,amani na usawa katika familia na jumuiya zetu, kwa mahitaji ya mwili na roho zetu, kwa yale ya ndugu, wafadhili na adui zetu.

Atukuzwe…
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu …

7. Ee Baba wa milele, tunakutolea Damu Takatifu ambayo Yesu alimwaga msalabani na kila siku anaitoa katika sadaka ya Misa, kwa wale watakaoaga dunia leo na kwa roho zilizopo toharani ili waungane na Kristo katika utukufu.

Atukuzwe.
Asifiwe na kushukuriwa milele Yesu…

"...Katika ninyi nakuta watu waliokombolewa, ambao kwa ajili yao Kristo alitoa damu yake.
Damu hii huwanenea ninyi kuhusu upendo usio na mipaka wa Baba na Mwanawe Yesu Kristo, upendo ulio kwa ajili yenu na kwa ajili ya watu wote; Damu hii ni chemchemi ya furaha ile iliyo kubwa kuliko zote za dunia, furaha ya kuweza kupenda na kufahamu kwamba tunapendwa. Damu hii inawapa nguvu inayohitajika kwa kuanza maisha mapya."

Papa Yohana Paulo II

KUJIWEKA WAKFU KWA DAMU YA YESU

Tunakushukuru, Bwana Yesu Kristo kwa kujifanya mtu na kuleta pendo la Baba wa mbinguni katika ulimwengu wetu. Tunakushukuru, Mwana wa Mungu, kwa kutwaa mwili na damu yetu, na kuwa ndugu na rafiki yetu. Tunakushukuru, mchungaji mwema, kwa kuutoa uhai wako kwa ajili ya kundi lako, ili kuwaosha na kuwatakasa wale wanaopokea neno lako na kuwa washiriki wa sadaka yako ya upatanisho.

Pamoja na malaika na watakatifu wote tunakusifu na kukutukuza, Ee Bwana, kwa kuondoa kosa la wanadamu kwa Damu yako Azizi. Tunakuheshimu na kukutukuza kwa kutupatia tumaini jipya kwa kutoa maisha yako: kifo kwetu sasa ni mlango wa ufufuko, na katika huruma uliyotuonyesha, tukiungana nawe, sisi nasi twaweza kuwa chanzo cha huruma na upatanisho.

Tunakusifu na kukutukuza, Mwokozi wetu, kwa kuwa kwa njia ya Ubatizo na Kipaimara unatufanya viungo vya mwili wako mtakatifu, yaani Kanisa; kwa njia ya Ekaristi Takatifu unatuunganisha katika muungano wa upendo na amani, na kwa njia ya Sakramenti ya Upatanisho unaponya majeraha yetu sisi tunaosafiri duniani, na kuturudishia upya maisha ya neema.

Tunakushukuru na kukutukuza, Ee Yesu, kwa Neno lako na Sakramenti zote, ambazo hutufanya viungo hai vya Kanisa.

Tunakushukuru kwa ajili ya wale wanaoongoza kundi lako ulilioliunganisha kwa Damu yako. Shukrani zitolewe kwako, Ee Bwana, kwa ajili ya wote waliotusaidia kupata imani, na kwa wale waliotuongoza katika njia ya pendo lako.

Tunakushukuru kwa namna ya pekee leo, kwa kuwa katika Damu yako tumegundua maana ya fumbo la maisha, mateso na kifo. Jinsi ulivyoshiriki maisha yetu kwa upendo, ukateswa na ukafa msalabani, hivyo nasi tunamtolea Mungu Baba pamoja nawe maisha yetu, mateso na hata kifo chetu, ili tuwapende ndugu zetu kama wewe ulivyotupenda sisi.

Kwa hiyo leo tunajitolea kwako, tuwekwe wakfu tena kwa njia ya Damu yako Azizi. Tunarudia upya ahadi za Ubatizo na tuna hamu ya kuimarika zaidi na kuwa zaidi viungo hai vya mwili wako, Kanisa. Tunataka maisha yetu yasaidie kukamilisha kile kinachopungua katika ukombozi na

wokovu wa ulimwengu. Tunapenda muda wetu uwe muda wako, furaha yetu iwe furaha yako, na mateso yetu yashiriki katika pendo lako la ukombozi. Pamoja nawe tuwe tayari kutoa damu yetu, na hata uhai wetu kwa ukombozi wa ulimwengu.

Ee Bwana, tujalie kuwa pamoja nawe chemchemi ya huruma, ili tushinde woga na roho mbaya; tuwape nguvu mpya waliopo hatarini au waliojeruhiwa; tuwafariji wenye huzuni; tuonyeshe njia ya ukweli kwa wanaoitafuta; tuwahimize wakosefu wakurudie; tuwaimarishe waliojitolea kwako; tuwahudumie wanaokufa na tuwaombee marehemu katika kujitakasa kwao.

Ee Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya Damu yako Azizi, utujalie kuishi kiaminifu katika tendo hili la kujiweka wakfu kwako. Utufanye waabudu wa fumbo la upendo wako. Utujalie nguvu ya kutoa ushuhuda wa wito wetu, ili watu wengi zaidi washiriki katika kuabudu Damu yako Azizi na kuungana nasi katika maisha ya kumtukuza Mungu na kujitolea kwa watu. Amina!

MISA YAKE NA YETU

Kama unateseka, na mateso yako jinsi yalivyo
yanakuzuia katika kila tendo,
kumbuka Misa.
Katika Misa, Yesu sasa kama wakati ule,
hafanyi kazi, hahubiri:
Yesu anajitoa mwenyewe kwa upendo.
Katika maisha
tunaweza kufanya mambo mengi na kusema maneno mengi;
lakini kwa sauti ya sikitiko,
hata kama haijasikika na kujulikana kwa wengine,
sikitiko linalotolewa kwa upendo,
ni neno lenye nguvu,
lenye kupenya mbingu.
Kama unateseka
unganisha mateso yako na mateso yake,
toa Misa yako mwenyewe;
na kama ulimwengu hautaelewa,
usihofu:
Inatosha kwamba Yesu, Maria na watakatifu
Wanakuelewa:
ishi nao,
na iache damu yako imwagike
kwa ajili ya binadamu.
Kama Yeye.
Misa!
Ni kuu kupita ufahamu wetu!
Misa yake na yetu!

Chiara Lubich

ROZARI YA DAMU AZIZI YA YESU

Rozari ya Damu Azizi ni moja kati ya mitindo ya kutafakari maisha ya Yesu. Katika kila fumbo, tunakumbuka tukio mojawapo la kumwaga damu katika maisha ya Mkombozi, alilotuonyesha kwa njia hii ya upendo wake.

Tendo lenyewe la kumwaga damu si kitu cha maana zaidi katika Rozari hii, bali ni njia ya kuunganisha pamoja, kama mnyororo, nyakati za unyenyekevu wa Mwana wa Mungu. Kama ishara ya kujinyenyekeza kwa Bwana wetu (Fil. 2:6-11), damu imekuwa alama yenye nguvu sana. Rozari huwaalika waamini kutafakari maisha ya Mkombozi anapomkomboa mwanadamu kutoka dhambini, kwa kujitwalia kwa hiari hali ya utumwa unaokubali mateso.

Hivyo, sala hii huonyesha shukrani, tumaini na uradhi katika kushiriki kwenye ukombozi uliopatikana kwa Yesu; na humpa kila mtu unyenyekevu wa kuwa tayari kumwaga damu pamoja naye. Jambo hili hutokea kiroho kila tunapoishi nyakati za masikitiko na za upendo. Imani katika Yesu Kristo leo yaweza kutudai sadaka ya afya, na ya maisha yetu kama ilivyotokea wakati wa mashahidi. Damu, kama alama ya maisha na ya sadaka iliyotolewa msalabani, imekuwa kwa wakristo onyesho la upendo wa Mungu. Damu ya Kristo kila mara ni kipimo cha upendo ule ambao Mungu hutudai. Inatubidisha kujiweka tayari kujitoa kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa wanadamu.

Rozari ya Damu Azizi ina alama katika fumbo lake na katika mfumo wake. "Baba yetu" hurudiwa mara thelathini na tatu kwa kutukumbusha umri wa Yesu alipotoa sadaka yake kuu. Mafumbo saba ya umwagaji damu hurejea utimilifu wa ukombozi. Namba zote mbili husisitiza kuwa maisha yote ya Bwana wetu yalilenga katika tendo lake la kutukomboa juu ya msalaba.

Rozari ya Damu Takatifu inaanza kama ifuatavyo:

Kiongozi (akifanya ishara ya msalaba anasema): Ee Mungu, uje kutusaidia

Wote: (wakifanya ishara ya msalaba huitikia): Ee Bwana utusaidie hima

Kiongozi: Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Wote: Kama mwanzo na sasa na siku zote na milele amina.

Kiongozi (Anataja fumbo).

Hufuata maneno ya Maandiko Matakatifu.

Hufuatiwa na tafakari ya Maandiko Matakatifu.

Baada ya tafakari hufuata sala.

Hufuata 'Baba Yetu' mara tano (5)

Mwisho wa kila fumbo humalizika kwa 'Atukuzwe Baba .....na kwa sala hii:

Kiongozi**: **Tunakusihi, Ee Bwana, uwasaidie wana wako,

***Wote: Uliowakomboa kwa Damu yako takatifu**.*

FUMBO 1

Yesu alimwaga Damu alipotahiriwa

"Siku nane baadaye, wakati wa kumtahiri mtoto ulifika. Wakampa jina Yesu. Jina ambalo alikuwa amepewa na malaika kabla hajachukuliwa mimba" (Lk. 2: 21).

Tafakari: Utii unaofanya huru

Kristo hakuja kutangua sheria za Agano la Kale bali kuzikamilisha; hivyo hakukanusha sheria ya zamani kwa nje, bali alijiweka chini yake ili aishinde kwa ndani. Hili linajionyesha wazi katika ibada ya kutahiriwa kwake. Kwa njia hii Yesu alipokelewa kuwa mtu wa Taifa la Israeli, kama vile sisi tunavyopokelewa katika Kanisa kwa kupitia ibada ya Ubatizo. Yesu alikuwa kama sisi katika kila kitu "isipokuwa hakuwa na dhambi." Ndiyo sababu alijiweka chini ya sheria ya Wayahudi. Lakini kwa njia ya upendo wake, Yesu anaweza kubaki huru, Yeye huuheshimu utii na huonyesha njia kwa wale wote wasiojisikia huru mbele ya sheria, mazingira, ibada na mapokeo.

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wale wote wasio huru katika mwili na roho. Kwa upendo wako uwajalie nguvu ya kuona sadaka yao kama njia ya kushiriki katika mwamko wa imani. Na wote watambue kwamba katika Damu yako Azizi, kila anguko linaweza kugeuka kuwa ushindi.

FUMBO LA 2

Yesu alimwaga Damu yake katika bustani ya Getsemane

"Yesu akiwa katika uchungu mkubwa, alisali kwa bidii zaidi; na jasho kama matone ya damu, likamtoka likatiririka mpaka chini" (Lk. 22: 44).

Tafakari: Ushindi dhidi ya woga

Huenda hatutapatikana na yale yaliyompata Yesu katika unyonge wake wa kibinadamu, alipokabiliwa na hofu ya kifo juu ya mlima wa Mizeituni. Kwa hiyo asiwepo mwenye kuona aibu ya kuogopa. Hata Mwana wa Mungu alihangaika alipokabiliwa na kifo. Mwinjili anatueleza kwamba jasho lake la hofu lilikuwa kama matone ya damu. Yesu alijeruhiwa mno na dhambi ya usaliti. Ubinadamu wake unataka kukwepa mateso, lakini upendo wake kwa Baba hushinda: "mapenzi yake yatimizwe, na sio yangu." Yesu anatuonyesha njia ya kushinda woga kwetu sisi tulio wanyonge na wapweke tunapokabiliwa na vishawishi. Kukubali mapenzi ya Baba kulimfanya Mwana wa Mungu

kuwa mshindi juu ya woga, hivyo kwa kujitawala aliweza kumkabili msaliti na kujitoa mwenyewe kwake.

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wale wote walionaswa katika woga na kukata tamaa. Uwaongoze wasitafute kamwe usalama katika nguvu zao au kwa watu wengine, bali katika kutimiza mapenzi ya Baba. Utuwezeshe kuwa tayari kukubali na kutimiza mapenzi hayo, ili tusibaki tumeelemewa na hofu za zamani wala za sasa na hata za wakati ujao.

FUMBO LA 3

Yesu alimwaga Damu alipopigwa mijeledi

"Hapo Pilato akawafungulia Baraba kutoka gerezani, lakini akamtoa Yesu asulibiwe" (Mt. 27: 26).

Tafakari: Yesu anakubali kutendewa bila haki.

Baada ya kusalitiwa na kukamatwa, Yesu anapelekwa mbele ya waamuzi mbalimbali. Mwishoni Pilato japo hajamwona kuwa na kosa anaamuru apigwe. Hakuna kinachomuumiza mwanadamu zaidi ya dhuluma au hukumu isiyo na haki. Haya maumivu ya kiroho yaliongezeka juu ya mateso ya mwili yaliyopatikana kutokana na mapigo aliyopigwa. Yesu alivumilia mapigo hayo kwa sababu ya dhambi za watu. Hakulalamika wala kukataa. Pendo lilimfanya aweze kuvumilia dhuluma na mateso; kweli pendo linakomaa kwenye hali ya namna hiyo!

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wale wote ambao wanashtakiwa kwa uwongo na kuhukumiwa bila haki. Zungumza nao kwa kutumia alama ya damu yako, na uwafanye waelewe kwamba, damu yao haitamwagika bure ikiwa sadaka yao inatolewa kwa Mungu. Utujalie kuelewa kwamba amani haipatikani kwa kutumia nguvu, bali huja baada ya kushiriki kikamilifu katika mateso ya Kristo.

FUMBO LA 4

Yesu alimwaga Damu alipovikwa taji la miiba

Wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamwekea kichwani. Wakaanza kumsalimu, "Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" (Mk. 15: 17-18).

Tafakari: Yesu alikubali dhihaka na hukumu ya dhuluma

Askari walimtendea Yesu vibaya zaidi kuliko walivyoamriwa. Siyo tu taji la miiba lililomwumiza, bali na madhihaka pia. Maumivu haya ni makuu kuliko yale ya mwili: yapenya hadi ndani ya roho. Hata hivyo wale wamtesao wasema kweli: 'Yesu ni mfalme' na kweli ni mfalme kwa kuwa kutoka kwake huja mamlaka yote. Kwa damu iliyotoka kwenye taji la miiba, Kristo ameutukuza mzigo wa wajibu. Kwa kushiriki utawala wa Kristo, mkristo hutawala kwa kutumikia, na kwa njia ya dhuluma anazozipata, hujiweka tayari kushiriki utukufu wa Bwana wake.

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wale wote wanaoteseka chini ya watu wenye mamlaka. Kwa Damu yako Azizi uwape hekima na nguvu wenye kushika nafasi hiyo. Baki karibu na wale wanaochukua mzigo wa wajibu kwa wengine. Utujalie tusiwe na hatia ya kuwalaumu bila upendo na hivyo tukuone wewe katika hao wenye madaraka**.**

FUMBO LA 5

Yesu alimwaga Damu katika safari yake ya kuelekea Kalvari

"Basi wao wakamchukua. Naye akatoka akiwa amejichukulia msalaba wake kwenda mahali paitwapo 'Fuvu la kichwa', kwa Kiebrania Golgotha" (Yoh. 19: 17).

Tafakari: Pendo lisilovunjika

Siyo maandamano ya utukufu na enzi aliyoyafanya Yesu alipoelekea Kalvari. Lakini hata hivyo ni ushindi, ni ushindi wa upendo! Yesu alianguka zaidi ya mara moja. Si uzito wa msalaba tu uliomwagusha, bali pia ubaya uliomzunguka na uchungu wa rohoni. Pendo la Yesu halikutetereka. Liliendelea kuimarika na kuangalia zaidi mateso ya wengine kuliko mateso yake, kama alivyofanya alipokutana na mama yake, alipomtuza Veronika zawadi ya picha ya uso wake kwenye kitambaa na alipowafariji wanawake wa Yerusalemu.

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wale ambao misalaba yao imekuwa mizito mno. Kwa Damu yako Azizi uwasaidie kusimama kila wanapoanguka katika majaribio ya maisha. Uwajalie wote watambue kwamba pendo la kweli laonekana katika ulimwengu huu tunapodumu katika safari yetu bila kurudi nyuma.

FUMBO LA 6.

Yesu alimwaga Damu aliposulibiwa

Mnamo saa tisa Yesu akalia kwa sauti kubwa: "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mt. 27:46).

Tafakari: Uaminifu katika kujitolea

Msalabani Yesu alisikia ugumu wa upweke. Mpaka wakati huu alipata kitulizo na msaada katika kuungana na Baba yake, kama katika mahangaiko ya Getsemane.

Sasa Mwana wa Mungu hasikii tena kitulizo hicho. Mungu anaonekana kuwa mbali.

Damu inapomtoka moyo wake unazimia. Yote yaonekana kuwa ni bure na maswali ya mateso yake hayana majibu.

Hata hivyo hakati tamaa: “Baba mikononi mwako naiweka roho yangu” (Lk. 23:46).

Huu ni ushindi wa imani, ushindi wa upendo unaoshinda yote.

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wote wasioona maana katika maisha yao na wale ambao wanafanana nawe msalabani kwa kusalitiwa au kuteswa.

Wajalie wapate nguvu katika Damu yako, ili wakati wa giza, wakiungana nawe, waweze kusikia pendo la Baba.

FUMBO LA 7

Yesu alimwaga Damu alipochomwa ubavuni kwa mkuki

“Walipomfikia Yesu waliona kwamba alikwisha kufa, na hivyo hawakumvunja miguu. Lakini askari mmojawapo alimtoboa ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji” (Yoh. 19:33-34).

Tafakari: Maisha kupitia kifo

Tendo la kuchomwa ubavuni lilieleweka tangu mwanzo na Kanisa kama chemchemi ya uhai wetu: maji ya ubatizo na damu ya Agano Jipya. Hata leo chemchemi hiyo yaendelea kupatikana katika sakramenti, hasa ya Upatanisho na Ekaristi.Sakramenti hizi zinatualika kukutana na Yesu msulibiwa na mfufuka ili tutakaswe toka dhambi zetu na tupate uzima mpya. Kwa kuwa bado tunaishi hapa ulimwenguni, tunatawaliwa na kifo; lakini kwa kifo chetu hatimaye tutaunganika na kifo na ufufuko wa Kristo. Ni zawadi ya pendo la Mungu, kwamba, katika kupokea

sakramenti, tunaweza kuanza tangu sasa kuunganika na Mungu pamoja na watakatifu wake!

Sala

Bwana Yesu, tunawaombea wote wasiokufahamu na wote ambao au kwa kujitenga na Kanisa au kwa sababu ya dhambi na makosa yao wamepoteza neema ya sakramenti.

Utujalie tupate katika Damu yako chanzo cha upatanisho na tuone ndani yake kiungo cha umoja na upendo.

Kule kupokea kwetu sakramenti, kwa moyo na ibada, kutuunganishe nawe na wengine na kutuwezeshe kuishi na kufanya kazi kwa ajili ya ufalme wako.

SALA YA MWISHO

Bwana Yesu, tumetafakari juu ya kumwagika kwa Damu yako. Ulijinyenyekesha kwa ajili yetu, ili kuondoa dhambi zetu na kutustahilisha utukufu wa kuitwa wana wa Mungu. Sisi tunakushukuru na kukuomba utujalie tuweze, pamoja nawe, kutoa damu yetu na maisha yetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu na wokovu wa jirani zetu.

Tunapokuwa katika huzuni au katika furaha, utusaidie kutafakari juu ya thamani ya ukombozi wetu na kuitikia pendo lako kwa ukarimu zaidi.

K: Astahili sifa na shukrani Yesu

W: Aliyetukomboa kwa Damu yake Takatifu.

NJIA FUPI YA KUSALI ROZARI YA DAMU TAKATIFU

Kiongozi (*akifanya ishara ya msalaba*):

Ee Mungu, uje kutusaidia

Wote: (*wakifanya ishara ya msalaba):*

Ee Bwana, utusaidie hima.

Fumbo la 1: Yesu alimwaga damu alipotahiriwa , (Lk. 1: 59)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Kiongozi: Tunakusihi, Ee Bwana, uwasaidie wana wako,

Wote: Uliowakomboa kwa Damu yako Takatifu.

Fumbo la 2: Yesu alimwaga Damu katika bustani ya Getsemane, (Lk. 22:44)

Baba yetu (mara 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Fumbo la 3: Yesu alimwaga Damu alipopigwa mijeledi, (Mt. 27:26)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Fumbo la 4: Yesu alimwaga Damu alipovikwa taji la miiba, (Yoh. 19:2)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Fumbo la 5: Yesu alimwaga Damu katika safari yake ya kuelekea Kalvari (Yoh. 19:17)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Fumbo la 6: Yesu alimwaga Damu aliposulibiwa, (Yoh. 19:18)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Fumbo la 7: Yesu alimwaga Damu alipochomwa ubavuni kwa mkuki, (Yoh. 19:31)

Baba yetu (*mara* 1) na Atukuzwe (*mara* 5)

Tunakusihi…

Sala ya mwisho

Bwana Yesu, tumetafakari juu ya kumwagika kwa Damu yako. Ulijinyenyekesha kwa ajili yetu, ili kuondoa dhambi zetu na kutustahilisha utukufu wa kuitwa wana wa Mungu. Sisi tunakushukuru na kukuomba, utujalie tuweze, pamoja nawe, kutoa damu yetu, na maisha yetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na wokovu wa jirani zetu.

Tunapokuwa katika huzuni au katika furaha, utusaidie kutafakari juu ya gharama ya ukombozi wetu na kuitikia pendo lako kwa ukarimu zaidi. Amina.

Kiongozi: Tunakuabudu, ee Yesu, na tunakutukuza.

Wote: Kwa kuwa uliukomboa ulimwengu kwa Damu yako Takatifu.

(Muundo wa kusali Rozari hii waweza kubadilika)*:*

Kwa mfano:

Unatangaza fumbo.

Unasoma sehemu ya Biblia.

Kila mmoja atafakari kwa muda mfupi.

Sala (Kama ilivyo katika Rozari ndefu)

NOVENA YA DAMU AZIZI

Ee Bwana Yesu Kristo, ulipopaa kwa Baba, siku arobaini baada ya ufufuko wako, uliwasihi mitume wangojee kwa pamoja Roho Mtakatifu. Walisali siku tisa kabla hawajapokea zawadi hiyo kubwa kuliko zawadi zote, na hivyo wakawa mitume.

Kwa hiyo, tukiamini kuwa hata leo utatupatia kilicho chema kwa wokovu wetu, tunasali:

Uziangazie akili zetu na utakase mioyo yetu, ili tujifunze kusali vizuri.

Ulisema, “Ombeni mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa,”(Mt:7:7) utushushie Roho uliyewapa mitume, tuweze kusali pamoja na Maria ambaye ni Bikira wa Bwana na mwombezi wetu katika kuomba.

Kwa mwaliko wa neno lako tunakuja kwako leo tukiomba kwa nia hii...(taja)

Yesu mwema, tunaamini katika pendo na huruma yako uliyotuonyesha katika Damu yako. Moyo wako daima uko wazi kwa maskini na wagonjwa, kwa wanaodharauliwa na wenye dhambi. Ulikausha machozi ya mjane wa Naim, ulimsikiliza akida na kuzawadisha imani ya Martha.

Utujalie sisi pia furaha ya kupata msaada wako na, kama maombi yetu hayaendani na mipango yako, uimarishe imani yetu kwa nguvu ya damu yako.

Pamoja nawe twasema: “Baba, mapenzi yako, siyo yangu, yafanyike!” (Lk: 22:24)

Utujalie kuamini kwamba njia zako ni sawa hata tunaposhindwa kuzielewa. Wewe ni upendo; na yote uliyotuletea na kuruhusu, yanatusaidia kufika kwenye wokovu wetu. Amina!

(*Pamoja na nia yako katika novena hii, unaweza kuongeza rozari ya Damu Takatifu*).

SHUKRANI YA WALIOKOMBOLEWA

Kweli ni vema na haki, wajibu wetu na ni chanzo cha uzima, kukushukuru daima na kila mahali wewe, Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyezi nguvu na wa milele, kwa Kristo, Bwana wetu.

Ulimtuma Kristo ulimwenguni huku, ili, kwa sadaka yake ya Pasaka mpya, awakomboe wanadamu wote kutoka kwenye utawala wa giza na, kwa kuwatakasa katika Damu yake Azizi, aunganishe pamoja kundi lililotawanyika.

Wote waliooshwa katika Damu ya Mwanakondoo, watamfuata na watashiriki utukufu wake usio na mwisho.

Kwa hiyo, tukiungana na malaika na watakatifu wote, twaimba wimbo wa utukufu wako bila mwisho.

“Amina, sifa, utukufu, hekima, shukrani, heshima, uwezo na nguvu kwa Mungu wetu milele na milele.”



KUSHIRIKI DAMU YA KRISTO

Sifa na shukrani ziwe kwako, Ee Bwana Yesu, unayetualika kula Mwili wako na kunywa Damu yako. Twaamini kuwepo kwako katika maumbo ya mkate na divai; katika fumbo hili hujenga upya Agano la milele la upendo wako na watu uliojipatia kwa Damu yako.

Tunatamani kuishi katika agano hili, tukiabudu zaidi na zaidi katika roho na kweli na kushuhudia kwa maisha yetu, nguvu ya Damu yako inayokomboa.

Uwajalie wote waliojitenga warudi karibu nawe kwa nguvu ya Damu yako, na kuta zote za utengano zikianguka, waungane nawe kuwa kitu kimoja katika Kanisa, mwili wako, lililozaliwa toka moyo wako uliotobolewa juu ya msalaba.

Ulijalie Kanisa lako, ambalo lapokea Damu yako, lipate roho yako ya upendo, kwa kupenda ulivyopenda wewe, kwa kukubali kikombe cha mapenzi ya Baba na kwa kuchukua msalaba unaokomboa.

Ee Yesu, endelea kutoa toka ubavuni mwako Damu na maji vitakavyoondoa dhambi zetu na kutusukuma, kwa kufuata mfano wako, kuwa wazi kwa ndugu zetu. Kule kupokea Mwili na Damu yako, kulifanye daima upya Kanisa lako na kuwajazia waamini wote furaha yako. Amina.

Bk. Maria Malkia wa Damu Azizi ya Yesu

SALA KWA MARIA, MAMA WA DAMU AZIZI

Tunakuheshimu Maria kwa kuwa Mungu amekuteua kati ya wanawake wote kuwa Mama wa Mwanawe. Kwake yeye, wewe ni kalisi safi na takatifu, kwa kuwa kwa njia yako ameiepusha dhambi ya asili, na pamoja nawe ameanzisha uumbaji mpya.

Unang'aa na kuangaza kwa usafi wa moyo wako. Wewe ni tunda la kwanza la ukombozi, ulioustahili kwa Damu ya Mwanao, hata kabla ya Yesu kuwa mtu ndani yako. Mungu amekutajirisha kwa njia ya pekee, ili uweze kutekeleza mpango wake bila kikwazo. Hivyo ulimkubalia kuwa Mama wa Mkombozi.

Bila kuweka masharti ulifuata hatua kwa hatua mapenzi ya Mungu kwa imani isiyotikisika. Ilikuwa njia ya majaribu, ya matukio yasiyotazamiwa, mwendo wa imani; hivyo ukajikuta mwenyewe juu mlima Kalvari, mbele ya Mwanao aliyetapakaa Damu, baada ya kufuatana naye maishani, na katika njia yake ya kuelekea msalaba.

Tunakupenda, ewe Mama chini ya msalaba, Mama wa Damu Azizi, kwa sababu mlimani Kalvari ulikuwa Mama yetu sote. Damu ya Yesu, iliyotoka kwako ulipompa mwili wa kibinadamu, ni damu ya ukombozi inayotiririka kutoka msalabani; hivyo wewe, Mama wa mwili wa Kristo, pia ni Mama wa Kanisa.

Tunatamani kukupenda wewe na Mwanao, na kukuheshimu kama Mwanao alivyofanya katika maisha yake, alipokuwa mtoto na mtu mzima. Pamoja naye tunapenda kushiriki maumivu yako na pia furaha zako. Mama, tuonyeshe namna tutakavyokupenda zaidi na hata kujisikia wanao na kukamilika ndani mwako zaidi.

Kwa kuwa Yesu alimwaga damu yake kwa ajili ya wote, hata moyo wako uko wazi kwa wenye matumaini, kwa waliotengwa, waliokata tamaa na wasiopendwa.

Tunataka kujiunga nawe Mama mwenye huruma kwa wote. Pamoja nawe twataka kutuliza na kusaidia binadamu, kwa kuwa wewe uko karibu hata na wale wasiokufahamu au kukuelewa.

Kaa karibu nasi, Mama wa Damu Azizi, ili tuwe karibu na hao unaowapenda sana. Tupatie imani yako, tukubali kuongozwa na Roho Mtakatifu, kama ulivyofanya wewe.

Utupatie unyenyekevu wako, ili tuwatumikie wale ambao Yesu alikufa kwa ajili yao. Tujalie msalaba wako, ili tuweze kuwa na huruma kama yako kwa wale wanaoishi bila neema.

Maria, Mama yetu, utusaidie kuchukua nafasi yako katika dunia hii, ili Yesu zaidi na zaidi apate kuishi kati ya watu na ufalme wake ukue. Utusaidie kufuata mfano wako ili tujitoe wenyewe pamoja na Damu ya Kristo, kwa utukufu wa Mungu Baba na kwa wokovu wa ulimwengu mzima. Amina.

SALA KWA MTAKATIFU GASPARI KUOMBA UPENDO KWA DAMU TAKATIFU

Ee Mtakatifu Gaspari, ulimpenda hivyo Bwana, hata ukamfuata katika njia yake ya msalaba. Kwako mateso na magumu ya maisha hayakuwa kikwazo, bali alama hakika, kwamba Mungu anatutakasa kwa njia ya hayo na kutuongoza kwenye utakatifu.

Wewe hukukata tamaa uliposumbuliwa na maumivu ya kimwili, woga na majaribu ya moyoni. Kinyume chake, uliinua macho yako kwa Bwana aliye juu ya msalaba. Ulililamini pendo la Mungu lililomiminwa kwetu kwa Damu ya Kristo.

Madonda ya Bwana yalikuwa makimbilio yako. Katika hayo ulipata amani, kitulizo na furaha ya moyo, uliyoyashiriki na wengine.

Ee Mtakatifu Gaspari, utusaidie kushiriki katika imani yako, matumaini na upendo wako. Tunakusihi mfano wako na maombezi yako vitujalie imani na pendo imara na la kweli kwa Damu ya Yesu, ambayo itatufanya zaidi na zaidi kuwa kama Kristo msulibiwa.

Tunatumaini kuutukuza huu “Mto wa Rehema” siyo kwa maneno tu, pia kwa maisha yetu yote, ili idadi kubwa ya watu iweze kupata raha ya kweli na utukufu wa milele. Amina!

SALA KWA MTAKATIFU GASPARI KWA AJILI YA KANISA

Ee Mtakatifu Gaspari, wewe ulilipenda Kanisa lililokuwa linateswa; na kwa jina la Yesu ulikubali kudharauliwa na kupelekwa kifungoni.

Tunakuomba uliombee Kanisa la leo; utusaidie kuelewa namna ya kuishi na kueneza habari njema ya Injili.

Utujalie tuungane nawe na mioyo yetu iwe na huruma kwa maskini na wanaosahauliwa. Utuombee ili tuongeze ndani yetu upendo wa Damu ya Kristo na tuwe tayari kutoa maisha yetu.

Tunamshukuru Mungu kwa matendo na mfano wako bora. Imarisha muungano wetu nawe ili tusielemewe na udhaifu wetu, bali tukomae zaidi katika wito, kwa ajili ya utukufu wa Mungu na wokovu wa ndugu zetu. Amina!

"***Katika ibada kwa Damu Takatifu twapata hazina ya hekima na utakatifu; ibada iliyo kitulizo chetu, amani na afya yetu.***"

Mt. Gaspari Del Bufalo.

Mt. Gaspar Del Bufalo – Mtume wa Damu Azizi ya Yesu

SALA KWA MTAKATIFU FRANSISKO XAVERI

Ee Mtakatifu Fransisko Xaveri, Kanisa lina mahitaji mengi leo. Watendakazi katika shamba la Bwana ni wachache; washambuliaji wa Kanisa ni wengi. Utuombee kwa Mungu tupate watumishi wengi, wenye wito wa kipadre na kimisionari, ambao kwa ushujaa wako tayari kueneza ufalme wa Mungu, na kutangaza habari za ukombozi tulioupata kwa mastahili ya Damu ya Mwanawe. Utuombee katika kiti cha enzi cha Mungu, ili wakristo popote duniani waweze kueneza Imani ya kweli kwa njia ya ushuhuda thabiti wa maisha na pendo la kikristo.

Tunaomba ujumbe wa pendo la Mungu, upenye katika nchi zote duniani.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, upendo wa Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mtakatifu, vituunganishe sote katika imani moja. Amina!

Mt. Fransisko Xaweri – Mlinzi wa Shirika

SALA KWA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS

Ee Mtakatifu Maria De Mattias, mtangazaji na mtume hodari wa Damu Takatifu ya Yesu. Uliyetumia maisha yako yote kwa kuvuta roho za watu, kwenye chemchemi ya neema inayotoka moyoni mwa Yesu Msulubiwa. Unijalie moto wa mapendo, kama ule uliogusa moyo wako na bidii kwa wokovu wa watu, uliokuwa lengo kuu na la pekee la maisha yako. Amina!

Mt. Maria De Mathias

SALA YA MTUMISHI WA MUNGU YOHANE MERLINI KWA AJILI YA SHIRIKA

Ee Yesu wangu, toka moyoni mwangu nakutolea shukrani kwa upendo wako mkubwa, kwa kuniita miongoni mwao hao wanaoishi na kufanya kazi katika mwamko wa Damu yako Azizi.

Ee Mungu wangu, nijalie niweze kutambua thamani ya neema hii uliyonipa. Wito huu ulionipa ni chemchemi ya neema zingine zote. Umeniita niache ndugu zangu, rafiki zangu na starehe nyingine za dunia. Uwe kiongozi wa moyo wangu, niambatane nawe daima. Nakuomba na kukusihi dhambi zangu zisiwe kizuizi cha kupata huruma yako.

Kwa msaada wa neema yako, naahidi kuwa mwema, mwaminifu na mtiifu katika kutimiza mapenzi yako katika kila jambo. Najua, utanifanya kuwa mtakatifu, kwa hilo usifiwe mara elfu. Maisha yangu yote ni yako, nayatolea yote kwako; nataka kuwa wako, unitendee unavyotaka.

Nakubali majaribu, usumbufu, uchungu, taabu, magonjwa na lolote litakalonipata. Ee Mungu unipe upendo mkubwa, niishi maisha ya kukupenda wewe daima, mpaka kifo changu.

Lakini Yesu, sisali kwa ajili yangu tu. Ninalo deni kubwa kwa shirika hili lililonikaribisha kunipokea na kunitunza. Ni kwa jinsi gani nitaweza kulitumikia inavyostahili! Ee Bwana lilinde na kuliimarisha listawishe, liwe na upendo na lidumu daima katika mwanga wa Roho wako Mtakatifu. Shirika lipate kuzidisha huduma zake popote pale linapohitajika. Mpe kila mwanashirika mahitaji yake ya kiroho na kimwili. Waongoze viongozi wake ili watimize mipango yako tu. Mwaga baraka nyingi kwa wafadhili wetu. Bariki kazi na mipango ifanywayo na shirika ili izae matunda kwa watu wote.

Nakutolea pia vyama na jumuiya zote zinazotoa heshima kwa Damu yako Azizi, ili kazi zao zizae matunda kwa ajili ya wote. Ee Damu Takatifu ya Yesu ongeza nguvu ya sala.

Maria Mtakatifu, kwa maombezi yako tutapata amani ya mwili na roho na maisha bora ya milele. Enyi malaika wote wa mbinguni, hasa malaika mlinzi wangu, fikisha maombi yangu kwa Yesu na Maria ili kwa huruma yao, yapate kusikilizwa. Mtakatifu Fransisko Xaveri, Watakatifu

wote wa mbinguni, liombeeni Shirika, wanashirika wote na mimi mwenyewe, Amina.

Mtumishi wa Mungu – Giovanni Merlini

SALA YA KUMWOMBEA MTUMISHI WA MUNGU YOHANE MERLINI KUTANGAZWA MTAKATIFU.

Ee Baba wa milele, tunaomba upendeleo wako kwa ajili ya mtumishi wako Yohane Merlini, ili atangazwe Mwenyeheri na Mtakatifu. Kwa heshima ya Damu Takatifu, tunaomba uweke katika maisha na kazi zake muhuri wa uthibitisho wa kimungu, ili wale wanaomheshimu na kuomba maombezi yake waweze kukutukuza wewe katika karama zake. Utujalie neema nyingi kutoka katika Damu ya Mwanao; uweke ndani yetu roho ya upendo wake, ili tuweze kweli kutangaza utukufu wako katika utume wa Damu Azizi kwa ujasiri kama Mtakatifu Gaspari na Mtumishi wako Yohane Merlini. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Maria Malkia na Mama yetu wewe unayeweza kutuombea kwa Mwanao, tunakuomba utuombee kupitia ukuhani mtukufu wa Kristo, upendeleo kwa ajili ya baba yetu mpendwa mwenye ari, Yohane Merlini aweze kutangazwa mtakatifu.

SALA KWA AJILI YA MAHITAJI YA SHIRIKA

Tusali kwa ajili ya shirika letu, kwa viongozi wake na wanashirika na kwa ongozeko la miito.

Ee Bwana, kwa maombezi ya Mtakatifu Gaspari na ya Mtakatifu Fransisko Xaveri, libariki Shirika letu, viongozi wake na wanashirika wote. Utujalie wanashirika wengi walio na ari ya kulitumikia shirika kwa unyenyekevu na utii, na katika kila kitu watangaze mapenzi yako.

Tusali kwa ajili ya Utume wetu.

Ee Bwana, ulisema: "Mavuno ni mengi lakini watendakazi ni wachache,"(Mt. 9:37). Chochea kati yetu miito mingi kwa ajili ya kazi za Kitume na Kimisionari na wabariki wale wote wanaotoa huduma hii. Watakatifu Mitume Petro na Paulo na wamisionari wote watakatifu wawasaidie na wawalinde wamisionari hao.

Tusali ili tuweze kutambua na kutekeleza utume wetu katika dunia ya leo.

Ee Bwana, tusaidie tutambue na tuwe tayari katika wajibu wetu. Utusaidie tuelewe alama za nyakati, ili kazi zetu za kitume zizae matunda kwa ajili ya wokovu wa watu na kwa utukufu wako.

Tusali kwa ajili ya wagonjwa.

Ee Yesu mwenye huruma, kwa neema zako waangalie watumishi wako ambao ni wagonjwa. Uwafariji na uwape nguvu. Pokea sala zetu kwa niaba yao, na wajalie kupokea mateso yao kwa moyo uleule uliokufanya upokee msalaba kwa ajili ya ukombozi wetu.

Tusali kwa ajili ya wafadhili wetu.

Ee Bwana, kwa wema wako wajalie maisha mema na yenye baraka wale wote wanaotutendea mema kwa ajili ya jina lako.

Tusali kwa ajili ya kuomba neema ya kifo chema.

Ee Yesu, mfalme wa utukufu wa milele, utujalie ili tuweze kuiacha dunia hii katika upendo wako, na utufikishe katika mwanga wako mtakatifu. Mtakatifu Yosefu, mwombezi wa wanaokufa, utuombee.

Tusali kwa ajili ya roho zilizoko toharani, hasa kwa ajili ya marehemu wetu wanashirika na wafadhili.

Raha ya milele uwape, Ee Bwana. Na mwanga wa milele uwaangazie.

K. Wapumzike kwa amani.

W.Amina.

HISTORIA FUPI YA MAISHA YA MTAKATIFU GASPARI DEL BUFALO

Katika nyakati za Mtakatifu Gaspari, Kanisa lilihitaji kufufuliwa upya kiimani. Mitafaruku ya kisiasa ilichafua sana cheo cha Upapa na vita vya mfalme Napoleone vilikuwa tishio kubwa kwa maendeleo ya Kanisa. Akiwa bado padre kijana, Gaspari alikataa kula kiapo cha kumtii Napoleone na akawapa wengine moyo wa kufanya vivyo hivyo. Zilitumika mbinu za kumvutia na kumshawishi Gaspari ili aape, lakini jibu lake lilifanana na majibu ya mashahidi wa kwanza: **"Siwezi, sipaswi, sitaki."** Akapelekwa kifungoni.

Kama mwanzilishi wa Shirika la Kimisionari, Gaspari aliamini kabisa kwamba mfuasi wa kweli wa Yesu anapaswa kujishughulisha kikamilifu na maisha ya watu na mahitaji yao.

Wito wa Gaspari ulijitokeza mwanzoni kabisa mwa maisha yake na ulikomazwa hadi upeo wa utakatifu na watu na mazingira aliyokutana nayo. Alizaliwa tarehe 6, Januari 1786 huko Roma Italia. Alipokuwa na miaka miwili alishikwa na ugonjwa wa ndui na akawa kwenye hatari ya kuwa kipofu. Mama yake Annuciata alimweka chini ya ulinzi wa Mtakatifu Fransisko Xaveri na kumwombea apone. Tukio hilo la kupona kwake lilimgusa Gaspari na katika utafiti likawa chanzo cha wito wake wa kimisionari. Pia maisha ya mtakatifu Fransisko wa Assisi yalimgusa Gaspari, hasa kazi aliyoifanya bila kuchoka, msimamo dhidi ya fahari za dunia na upendo kwa viumbe vyote vya Mungu. Wito wake wa kimisionari, ndani na nje ya nchi yake, ulijengeka juu ya mifano ya watakatifu hawa. Mafungo na mahubiri yake yalielezwa mara nyingi kama ***"tetemeko la kiroho,"*** kwenye mioyo ya wasikilizaji wake kwa kuwa, baada ya hayo, wengi walipata mtazamo mpya wa maisha.

Mama Bikira Maria alichukua nafasi ya pekee katika maisha na kazi za Mt. Gaspari. Tarehe 15 Agosti 1815, sikukuu ya kupalizwa Bikira Maria mbinguni, Shirika la Damu Takatifu ya Yesu lilianzishwa, na Gaspari akaliweka chini ya ulinzi wake.

Katika safari na mahubiri yake Gaspari alikuwa akichukua picha ya Bikira Maria inayojulikana kwa jina la "Mama wa Damu Azizi."

Mtu mwingine ambaye alimgusa Gaspari ni rafiki na mwungamishaji wake wa maisha, padre Albertini. Sista Maria Agnesi, aliyeishi maisha ya utakatifu, alitabiri hivi kwa padre huyu: "Utakutana

na padre kijana mwenye ibada ya pekee kwa Mtakatifu Fransisko Xaveri. Lengo lake litakuwa kufufua utume wa kimisionari na ataanzisha jumuiya ya mapadre na masista chini ya mwamko wa Damu Azizi. Kwa njia yake Mungu atarudisha watu kwenye uongofu wa maisha, atawapa mwamko mpya mapadre wa jimbo na kuwageuza wasioamini na waliokata tamaa kwenye pendo na imani ya Kristu msulibiwa."

Nyakati za Gaspari zilikuwa ngumu sana. Italia ilikuwa imechafuliwa na mawazo ya kupinga ukristo; ilijaa vikundi vya siri vya kisiasa; zaidi ya hayo wizi wa nguvu barabarani ulizidi. Papa Pius VII alimwomba Gaspari asafiri kote katika rasi ya Italia kwa kushiriki katika marekebisho ya dini na maadili. Gaspari alikubali na alichukua mpango huu kama lengo na sababu ya maisha yake pamoja na wenzake.

Mara Shirika lake lililokuwa linaanza kukua lilibarikiwa na Baba Mtakatifu Pius VII na nyumba ya misioni ya kwanza ilifunguliwa huko *San Felice*, karibu na Assisi. Hapa, chini ya anga la Assisi, mahali ambapo Fransisko wa assisi alisikia maneno ya Yesu na aliyaishi, Gaspari alielewa pendo la Yesu katika tendo la kumwaga Damu na kusukumwa kueneza Ibada hii, ambayo Papa Yohane XXIII aliita, "Ibada ya wakati wetu."

Wakati kazi zake za kitume zikiendelea kwa kasi kabisa, matatizo na masumbufu nayo yaliongezeka. Baadhi ya watu walishangaa jinsi Gaspari alivyoweza kukaa kimya aliposhtumiwa kwa uwongo. Jibu lake lilikuwa: ***"Kazi ni ya Bwana yeye anajua jinsi ya kuiendeleza."*** Hata matatizo yalipohatarisha usalama wake, jibu lake halikubadilika: ***"Lengo langu ni kuteseka, kusali na kukaa kimya."*** Hakusita kuwashauri wamisionari wake kutumia mtindo huo katika matatizo.

Mara kwa mara alama za nguvu ya Mungu ziliimarisha kazi yake ya kitume. Hata Papa Leo XII alimpa moyo wakati mmoja alipomkumbatia na kusema: "Mwanangu, una maadui wengi, lakini usiogope, Papa yu pamoja nawe."

Hata kule kukutana na Maria De Mattias kulikuwa baraka iliyozaa matunda mengi. Gaspari alitambua kwamba Mungu alikuwa na mpango maalum kwani huyu angeweza kuanzisha jumuiya ya watawa ambao wangefanya kazi bega kwa bega pamoja na wamisionari wake. Tangu lilipoanzishwa, shirika la Masista "Waabuduo Damu ya Yesu,"

limesambaza huduma zake ulimwenguni kote. Huduma zao za kitume zimeenea ulimwenguni.

Utume wa Kimisionari ambao ndiyo chanzo na lengo la kazi za kitume za Gaspari uliendelea kupanuka na kuongeza mambo mengine. Vipindi kati ya misioni moja (yaani uinjilishaji wa kina kwa watu wote) hadi nyingine vilijazwa na mafungo mbalimbali ya kiroho kwa mapadre, masista, wafungwa, wafanyakazi, wasanii na vikundi vingine. Gaspari alijishughulisha sana katika kutoa miongozo kwa Shirika lake changa hususani kuandika Katiba ya Shirika, kutunga sala mbalimbali za shirika na kuongoza mafungo. Kule kurudi kwake Roma mara kwa mara kulimpa nafasi ya kuimarisha kazi alizozianzisha katika ujana wake na ambazo bado alizipenda: Chuo cha Mtakatifu Galla kwa wasiojiweza na maskini, Oratori ya Mtakatifu Maria *in Vincis* (Maria Mshindi) kwa wafungwa na mapadre wazee na jumuiya ya Damu Takatifu ya Yesu kwa ajili ya walei. Wanashirika wenzake waliona ugumu wa kazi hizi kwa afya yake na mara kwa mara walikuwa wakimshauri apumzike kidogo. Jibu lake linaonyesha moto uliokuwa unawaka ndani mwake: ***“Kwa Mungu ni lazima tufanye mengi, upesi na vizuri; mengi kwa sababu anastahili hivyo, upesi kwa sababu maisha ni mafupi, na vizuri kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kumtumikia Mungu.”***

Daima alitoa sadaka na kufanya kazi njema, akawa mfano wa mtumishi mwema na mwaminifu wa Mungu ambaye alitolea kwa uwezo wake wote vipaji vyake kwa manufaa ya watu.

Kwa Mt.Gaspari Ibada kwa Damu Azizi ya Yesu ilikuwa ndiyo kiini halisi cha imani. Daima alisisitiza juu ya Ibada hii kuwa ***"Ni njia salama ya kuufikia utakatifu wa binafsi, chachu ya maisha mapya ya jumuiya na nguvu imara ya kazi ya kitume.”***

Siku hizi mafundisho ya Kanisa yatokanayo na Mtaguso Mkuu wa pili wa Vaticano yanasisitiza sana juu ya Fumbo la Damu ya Ukombozi ambayo ni chanzo cha neema zote zinazotufikia kwa kupitia Liturjia ya Fumbo la Pasaka. Litania za Damu Azizi ya Yesu, ambayo ni sehemu ya sala za Shirika, iliidhinishwa na kuenezwa kwa Kanisa zima na Mwenye Heri Papa Yohane XXIII. Mtaguso Mkuu wa pili wa Vaticano uliwekwa chini ya ulinzi wa Mtakatifu Gaspari. Mwenye Heri Papa Yohane XXIII alimtangaza Mt.Gaspari kama “Mtume mkuu na wa kweli aliyeeneza ibada kwa Damu Azizi ya Yesu ulimwenguni kote.”

Nia ya Mt. Gaspari bado ni hai katika wafuasi wake--mapadre, wamisionari, mabruda na masista wa Damu Azizi ya Yesu--ambao kazi zao zimeenea ulimwenguni. Kwa maisha na majitoleo yao, hufanya fumbo la Damu ya Yesu--Damu ya upatanisho na amani--ipenye mahali pote waendapo.



Mwenye Heri Papa Yohane XXIII

HISTORIA FUPI YA MAISHA YA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS

Mungu alifufua katika Kanisa Shirika la Masista Waabuduo Damu Takatifu ya Yesu kwa njia ya maisha na karama ya Mtakatifu Maria De Mattias, mwanzilishi wa Shirika hilo.

Mt. Maria De Mattias alizaliwa na kubatizwa Valecorsa Italia, tarehe 4.2.1805. Alilelewa katika familia iliyokuwa na msingi bora wa kikristo ambapo alijifunza kusali na kuwahudumia majirani.

Katika ujana wake alisikia wito wa pekee wa kumfuata Yesu msulubiwa kwa karibu zaidi na hivyo kuweza kujitoa kwake kwa upendo.

Akiongozwa na Mt. Gaspari, mwanzilishi wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi, Mt. Maria De Mattias alitambua polepole kwamba Mungu alikuwa amemzawadia karama ya kuanzisha Shirika la Masista.

Msingi wa Shirika hili ni upendo, na utume wake ni kushiriki katika kazi ya ukombozi kwa njia ya utumishi kati ya maskini na waliosahauliwa. Maria De Mattias aliitikia wito huo alipofungua, nyumba yake ya kwanza kijijini Acuto, karibu na Roma, tarehe 4. 3. 1834.

Alijituma katika kazi ya uongozi wa Shirika kwa nguvu zake zote kwa ajili ya Kanisa. Aliongoza Masista wake katika utakatifu, alifanya kazi ya kitume kati ya watu wenye mahitaji.

Baada ya kuugua kwa muda mrefu alifariki mjini Roma tarehe 20.8.1866. Alitangazwa Mtakatifu na Papa Yohane Paulo II, tarehe 18. 5. 2003. Leo hii shirika la Masista waabuduo Damu Takatifu ya Yesu wameenea ulimwenguni.

Wakiitwa na kutumwa kuishi na kuonyesha upendo wa Yesu, unaomwabudu Baba na kuwakomboa watu wote, Masista waabuduo Damu Takatifu wanashirikiana na Yesu katika kujenga mwili wake kwa njia mbalimbali za uenezaji wa dini na maendeleo kufuatana na mahitaji ya mahali walipo.

BABA YETU

Wewe uliniumba kwa mpango,
na kwa kazi pekee
Kwa ajili ya Kanisa na Ulimwengu.
Wewe daima ulifahamu ni kazi gani ninayoweza kuifanya,
mimi, na si mtu mwingine.
Nisipoikubali, haitafanyika;
ndio sababu nina kazi pekee ya kufanya.
Nifunulie maisha yako, nami nitakufuata.
Najua kwamba naweza kila kitu, nikiwa nawe, mwamba wangu.

Mungu anahitaji watu hodari kama Mt. Gaspari kufanya ulimwengu uwe mwema zaidi.

Ukitaka kujua zaidi kuhusu shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu lililoanzishwa na Mt Gaspari, andika kwa:

Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu,
Makao Makuu
S.L.P 932,
Dodoma
Simu. 026-2353097
Fax. 026-2353038
E- mail secretary@cppstanzania.com
AU tzvicariate@yahoo.co.uk

MANENO YA USHUHUDA

"...Ibada kwa Damu Takatifu ya Yesu kwa kweli ipo katika kiini cha maisha ya kikristo: Damu Azizi ya Bwana wetu ilikuwa daima kitu cha kupewa heshima maalum kwa upande wa watakatifu wote; ni shule ya utakatifu, haki, na upendo. Damu ya Kristo si fidia ya dhambi tu, wala ya kurudishia haki peke yake, bali, zaidi ya hayo, ni ufunuo wa huruma nyingi na pendo lisilo na kipimo. Hiyo husimika tena utu wa binadamu uliodhoofishwa na dhambi, na pia huinua hadhi ya mtu mpaka katika 'ushiriki katika asili ya kimungu.' Ndugu zangu, msiache kamwe kuchunguza ukweli huo juu ya fumbo hili la haki na upendo: mlieneze ulimwenguni kote."

Yohane Paulo II



Mtumishi wa Mungu – Papa Yohane Paul II